



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA UCHUKUZI
NATIONAL METEOROLOGICAL TRAINING CENTRE
CHUO CHA HALI YA HEWA
KIGOMA



SIMU : + 255 (0) 28 2988148
NUKUSHI : + 255 (0) 28 2988149
BARUA PEPE : nmtc@meteo.go.tz
Website: www.meteo.go.tz

(Kimepewa Ithibati kamili na NACTE)

**NAFASI YA KUJIUNGA NA MASOMO KATIKA NGAZI
CHETI KWA MWAKA WA MASOMO 2017/2018**

Chuo cha **Hali ya Hewa Kigoma** kipo chini ya WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILINO, kina uzoefu wa zaidi ya miaka arobaini (40) katika kufundisha wataalamu wa Hali ya Hewa.

Chuo kimepewa ithibati kamili na Baraza la Taifa la Mafunzo ya Ufundi (NACTE) kutoa mafunzo katika ngazi ya cheti na Diploma (NTA level 5 - 6) katika mfumo wa umahiri (CBET)

Chuo kinakaribisha maombi kwa waombaji wenye sifa kuomba kusoma Cheti katika Mambo ya Hali ya Hewa kwa mwaka wa masomo 2017/2018. Ada zetu ni nafuu kabisa.

SIFA ZA KUJIUNGA

Mwombaji awe amemaliza kidato cha sita (Form VI) na awe amefaulu masomo ya **Fizikia**, na **Hisabati** katika kiwango cha ufaulu wa 'Principal pass' kwa masomo yote mawili; ama 'Principal pass' moja na 'Subsidiary' moja.

NAMNA YA KUTUMA MAOMBI

Waombaji wote wenye sifa wanatakiwa kutuma maombi yao kwa njia ya mtandao kupitia mfumo wa NACTE;

<http://www.nacte.go.tz/Central Admission System>. Kwa maelezo zaidi tembelea tovuti ya NACTE: <http://www.nacte.go.tz>

AU;

Wajaze fomu ya maombi na kuituma Chuoni moja kwa moja.

Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 15/8/ 2017 saa 9:30 alasiri.

Masomo kwa mwaka wa masomo 2017/2018 yataanza Oktoba 2017

NB:

Kwa wale watakaotuma fomu za maombi yao Chuoni, waambatishe vivuli vya vyeti vya kidato cha nne na cha sita pamoja na nakala halisi ya hati ya malipo ya benki (Paying Slip) yenye kiasi cha Tshs. 20,000/= na ilipwe kwenye akaunti ya Bank -NMB (**DIRECTOR GENERAL, TANZANIA METEOROLOGICAL AGENCY Account number 20101000013**).

Fomu za maombi zitumwe kwa:

**Mkuu wa Chuo,
Chuo cha Hali ya Hewa,
S. L. P 301,
Kigoma-Tanzania**